# HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU

## TAARIFA YA MAPITIO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2014/15, 2015/2016 NA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA 2016/2017

### 1. Mapito ya bajeti ya mwaka 2014/15

(a) Katika kipindi cha mwaka 2014/2015 Halmashauri ilipanga kukusanya na kupokea jumla ya Tshs. **31,646,006,594** kwa kutekeleza Shughuli mbalimbali za maendeleo na matumizi ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2015 jumla ya Tshs. 29,287,578,109 zilikusanywa kutoka vyanzo mbalimbali. Aidha fedha zilizokuwa zimevuka mwaka ilipofika mwezi Juni 30, 2015 zilikuwa ni Tshs. 107,545,157. Fedha hizi zimeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/16.

**Machanganuo wa fedha za mwaka 2014/15**

| Chanzo cha fedha | Makisio 2014/2015 | Mapato halisi 2014/2015 | % |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 20,898,215,000 | 22,611,680,274.92 | 108 |
| Matumizi mengineyo | 1,986,833,500 | 1,241,352,362.85 | 62 |
| Miradi ya maendeleo na Wahisani | 4,311,419,000 | 3,906,834,635 | 90 |
| Mapato ya ndani | 1,754,562,000 | 926,967,429.07 | 53 |
| **Jumla kuu** | **28,945,840,500** | **28,686,834,700.92** | **99** |

**(b) Mapitio ya bajeti ya mwaka 2015/16**

Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 Halmashauri ilipanga kukusanya na kupokea jumla ya Tshs. **33,952,550,000** kwa kutekeleza Shughuli mbalimbali za maendeleo na matumizi ya kawaida. Mchanganuo wa mapato hayo ilikuwa kama ifuatavyo:-

| Chanzo cha fedha | Makisio 2015/2016 | Mapato halisi hadi Novemba 2015/2016 | % |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 27,111,250,000 | 14,180,840,684 | 52 |
| Matumizi mengineyo | 1,932,951,000 | 646,585,000 | 33 |
| Miradi ya maendeleo na Wahisani | 2,942,613,000 | 2,976,284,852 | 101 |
| Mapato ya ndani | 1,789,500,000 | 589,395,918 | 33 |
| **Fidia ya vyanzo vilivyofutwa** | **176,236,000** | **58,917,000** | **33** |
| **Jumla kuu** | **33,952,550,000** | **18,425,971,358** | **54** |

**Mchanganuo wa Mapato na Matumizi Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2015/16.**

| NA | MIRADI/ PROGRAMMU | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA ILIYOPOKELEWA 2015/2016 | MATUMIZI YA FEDHA ZOTE 2015/16 | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | RUZUKU YA MAENDELEO (LGCDG) | 1,033,274,000 | 0 | 0 | 2 |
| 2 | MPANGO WA MAENDELEO YA ELIMU SEKONDARI (SEDP) | 93,383,000 | 320,398,391 | 0 | |
| 3 | PROGRAM YA MAENDELEO YA MAJI (WSDP) | 75,277,000 | 704,084,000 | | 18 |
| 4 | MFUKO WA PAMOJA WA AFYA (HBF) | 433,824,000 | | | |
| 5 | MFUKO WA TUME YA TAIFA YA KUDHIBITI UKIMWI (TACAIDS) | 16,871,000 | | | |
| 6 | UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MAJI MAGU MJINI (MAOMBI MAALUM) | 400,000,0000 | | | |
| 7 | MFUKO WA BARABARA (ROAD FUND) | 503,230,000 | 868,668,704 | | |
| 8 | MIRADI ITOKANYO NA MAPATO YA NDANI (OWN SOURCE) | 1,076,049,000 | 24,000,000 | 24,000,000 | 2 |
| 9 | MFUKO WA KUENDELEZA NGOZI | 10,415,000 | | | |
| 10 | MFUKO WA JIMBO | 51,884,000 | | | |
| 10 | ULINZI NA USALAMA WA MAENDELEO YA WATOTO | 30,909,000 | | | |
| 11 | MRADI WA UJENZI WA JENGO LA OFISI ZA HALMASHAURI | 600,000,000 | | | |
| 12 | MRADI WA UJENZI WA NYUMBAZA WATUMISHI (W) | 200,000,000 | | | |
| **JUMLA KUU** | | **4,521,843,000** | | | |

**Mchanganuo wa Matumizi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo mwaka 2014/15(BAKAA)**

| NA | MIRADI/ PROGRAMMU | BAKAA 2014/2015 | MATUMIZI YA FEDHA ZOTE ZA BAKAA 2014/15 | % |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MIRADI YA KILIMO (DADPS) | 49,446,428 | 49,446,428 | 100 |
| 2 | RUZUKU YA MAENDELEO (LGCDG) | 196,000,786 | 0 | 0 |
| 3 | UNICEF | 44,181,152 | 44,181,152 | 100 |
| 4 | NYUKI | 649,400 | 0 | 0 |
| 5 | JENGO LA HALMASHAURI | 13,640,634 | 0 | 0 |
| 6 | MFUKO WA WANAWAKE | 14,054,926 | 0 | 0 |
| 7 | MPANGO WA MAENDELEO YA AFYA (MMAM) | 20,564,551 | 0 | 0 |
| 8 | IICD | 295 | 295 | 100 |
| 9 | MFUKO WA PAMOJA WA AFYA (HBF) | 507,195 | 507,195 | 100 |
| 10 | DRWSS | 34,782,465 | 32,215,280 | 94 |
| 11 | MFUKO WA BARABARA (ROAD FUND) | 3,608,908 | 3,608,908 | 100 |
| 12 | SEDP | 34,952,461 | 34,952,461 | 100 |
| 13 | DASIP | 48,719 | 48,719 | 100 |
| 14 | PATH FAINDER | 4,194,768 | 4,194,768 | 100 |
| 15 | AIDS RELIEF | 60,119,123 | 60,119,123 | 100 |
| 16 | MULTISECTORAL (TACAIDS) | 15,123,101 | 15,123,101 | 100 |
| 17 | UJENZI WA OPD HOSPITAL YA WILAYA | 100,000,000 | 0 | 0 |
| 18 | UJENZI WA CLINIC MIFUPA HOSPITAL YA WILAYA | 3,157,050 | 3,157,050 | 100 |
| 19 | UJENZI WA MAABARA | 29,842,596 | 0 | 0 |
| **JUMLA KUU** | | **534,874,558** | **247,554,185** | **46** |

## (c) 2.2 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KWA MWAKA 2014/15.

### SEKTA YA MAJI

- Ujenzi wa mradi wa maji bomba Nyanguge –Muda ulikamilika kwa asilimia 100
- Ujenzi wa mradi wa maji bomba Lugeye -Kigangama umetekelezwa kujengwa kwa asilimia 85

- Uchimbaji wa visima virefu 41na kufunga pampu za mikono umekamilika na unatoa huduma ya maji afi na salama katika kata za Magu mjini, Kitongosima,Kahangara kisima,Nyanguge,Bujashi,Lutale,Sukuma,Ng'haya na Nyigogo

- Ukarabati wa visima 29 ulifanyika katika kata za Kitongosima,Kahangara kisima,Nyanguge,Bujashi,Lutale,Sukuma ,Ng'haya,Bukandwe,Jinjimili ,Shishani na Nyigogo.

- Ujenzi wa nyumba ya mhudumu wa mitambo ya maji mradi wa maji bomba Lugeye-Kigangama.

- Ujenzi wa mradi wa umeme kutoka Lugeye hadi chanzo cha maji mradi wa maji bomba Lugeye-Kigangama.

**MIFUGO NA UVUVI**

- Kuongeza ubora wa nyama kwa walaji na mazao yatokanayo na mifugo kwa ujenzi wa Machinjio ya kati katika Magu Mjini.
- Kuongeza kipato cha wafugaji kwa Ununuzi na ufungaji wa mzani mmoja wa kupimia Ng'ombe,Mbuzi na Kondoo katika Mnada wa Kabila.
- Kupunguza vifo vya wanyama (Ng'ombe) vitokanavyo na magonjwa yanayoambukizwa na kupe kwa kutoa chanjo ya Ndigana kali (East Coast Fever) kwa ng'ombe 102 katika kata ya Magu Mjini.
- Kuongeza ubora wa koo saafu za mifugo(ng'ombe) kwa wafugaji wa Wilaya ya Magu kwa kuanzisha Vituo viwili (2) vya Uhamilishaji wa ng'ombe(Magu Mjini na Lugeye) na ununzi wa vifaa vya Uhamilishaji (Artificial Insermination kits).
- Kuwezesha wafugaji kumi (10) wa Wilaya ya Magu kushiriki kwenye maonesho ya nanenane kwa mwaka 2014 yaliyofanyika katika viwanja vya Nyamhongolo jijini Mwanza ambapo Halmashauri ya Magu ilipata nafasi ya kwanza katika kanda na mshindi wa jumla kwa Mfugaji bora kwa mwaka 2014.
- Kupunguza magonjwa ya mifugo na magonjwa yanayoathiri mifugo na binadamu ambapo jumla ya Mbwa 7,390 walichanjwa dhidi ya ugonjwa hatari wa kichaa cha Mbwa, Ng'ombe 7,200 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa chambavu (BQ), kuku 122,360 walipatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa wa mdondo na kuku 8,009 walipatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa wa Gumboro. Jumla ya mbwa 34 wazururaji waliuwawa katika kata za Kahangara,Magu Mjini na Ng'haya.
- Kuimarisha mtaandao wa wafugaji wa Wilaya ya Magu kwa kutoa mafunzo mbalimbali kwa wafugaji kwa Vikundi viwili (2) juu ya Ufugaji bora na wenye tija ambapo wanakikundi watano (5 ) wa vikundi vya Igunanilo

toka kijiji cha Nyanguge walihudhuria mafunzo ya ushonaji wa viatu na bidhaa nyingine zitokanazo na ngozi katika chuo cha DIT tawi la Mwanza.

**ELIMU SEKONDARI**

- Asilimia 58 ya watumishi wa Elimu sekondari walilipwa stahili zao ambazo ni fedha za likizo na uhamisho.
- Mitihani ya kidato cha pili, Kidato cha nne na Kidato cha sita ilifanyika kama ilivyopangwa.
- Ujenzi wa nyumba za walimu 2 na madarasa 4 ulikamilishwa.
- Walimu katika idara ya Elimu Sekondari wameongezeka toka walimu 427 kwa mwaka 2013 hadi walimu 516 kwa mwaka 2014. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 17.2.
- Ukamilishaji wa Hosteli nne katika shule za Magu na Lugeye
- Vyumba 46 vya maabara katika shule 8 za sekondari vilikuwa vimefikiwa hatua mbali mbali ya ukamilishaji
- Walimu 106 wamepandishwa madaraja,walimu 27 wamethibitishwa kazini na walimu 6 wamebadilishiwa muundo wautumishi.

**SEKTA YA AFYA**

- Haki za watumishi wa afya 120 zimetolewa kwa asilimia 80%
- Vifo vya kina mama wajawazito vimepungua kutoka 137/100,000 hadi 131/100,000.
- Vifo vya watoto vimepungua kutoka 10/1000 hadi 8/1000.
- Upatikanaji wa dawa ulifikia 68%
- Huduma za afya zimeboreshwa kwa kutoa kinga na tiba kwa ajili ya magonjwa mbalimbali ambapo (Utoaji Chanjo umefikia 95%
- Uendelezaji wa ujenzi wa vituo vitatu vya afya katika kata za Makuru, Mitundu na Itigi. Pia ujenzi wa zahanati tatu katika vijiji vya Ntope, Igwamadete na Rungwa

**ELIMU MSINGI**

- Uandikishaji wa Elimu awali- walikuwa ni wasichana ni 5,699 na wavulana 5,565 jumla 11,264 sawa na asilimia 89.2 ukilinganisha na waliotarajiwa 12,634.
- Uandikishaji wa darasa la kwanza - walikuwa ni wasichana 6,744 na wavulana 6,698 jumla 13,442 sawa na asilimia 98.9 ikilinganisha na waliotarajiwa 13,588.
- Uandikishaji wa MEMKWA - walikuwa ni wasichana 156 na wavulana 162 jumla 318 sawa na asilimia 64 ukilinganisha na waliotarajiwa 334
- Waalimu waliopo masomoni ni 62 wakiwa wanaume ni 29 na wanawake 33
- Walimu wa darasa la 1&11 wapatao 220 wamejengewa uwezo kwa kupata mafunzo ya ufundishaji wa KKK.

**MIPANGO TAKWIMU NA UFUATILIAJI**

- Mafunzo ya PLANREP yametolewa kwa watumishi 8
- Kamati za Maendeleo za Kata zimejengewa uwezo katika kusimamia miradi ya maendeleo

- Usimamizi na ufuatiliaji wa Miradi katika kata 25 umefanyika.
- Vijiji 82 viliwezeshwa kuibua viapaumbele vyao kupitia Mfumo wa Fursa na Vikwazo (O & OD).

**KILIMO NA UMWAGILIAJI**

- Uanzishaji wa vikundi 4 vya kilimo na mtandaowa wakulima katika vijiji vya Igekemaja na Shishani
- Wakulima 480 wamepatiwa mafunzo juu ya kilimo bora cha zao la mpunga na pamba.
- Mashine 2 za kisasa za kukoboa mpunga zimenunuliwa kwa ajili ya vikundi 4 katika vijiji vya Shishani na Ngasamo.
- Power Tiller 8 zimenunuliwa kwa ajiliya vikundi 8 vya wakulima wa zao la mpunga.
- Vikundi 4 vya wakulima vimepata mafunzo juu ya uzalishaji wa mbegu ya viazi lishe katika vijiji vya Isangijo na Chabula.
- Wajumbe wa serikali za vijiji 5 wamepata mafunzo juu ya usalama wa chakula (Food Security) katika vijiji vya Ilungu na Kahangara.
- Tumeshika nafasi ya kwanza kikanda katika maonesho ya wakulima NaneNane kwa mwaka 2014 yalifanyika viwanja vya NaneNane Nyamohongholo Mwanza
- Upatikanaji wa Kizima moto,mzani na kifaa cha kupima unyevu wa mazao (Hydrometer umefanyika umefanyika katika kijiji cha Igekemaja.
- Ujenzi wa tanki la kuvunia maji ya mvua na uwekaji wa solar umefanyika kwenye soko la kijiji cha Lutale na Ihayabuyaga.

.

**ARDHI NA MALIASILI**

- Miti 746,234 imepandwa, ambapo kati ya miti hiyo 234,543 ilipandwa na watu binafsi na miti 511691 ilipandwa na taasisi za serikali kwa maana ya mashule na magereza

- Doria imeimarishwa katika vijiji 19 vilivyopakana na hifadhi ya msitu wa Sayaka, hii ni sawa na wastani wa asilimia 40 kati ya doria zilikuwa zimepangwa kufanyika doria 2 kila mwezi.
- Doria 21 zimefanyika ili kupambana na uharibifu wa mazingira hasa kwa kuzuia uchomaji wa mkaa.Doria hizi zimefanyika katika vijiji vinavyozunguka hifadhi ya Sayaka yaani Mwabulenga, Sayaka, Bibinza, Mtaa wa Mwabasabi, Lubugu na Misungwi.
- Jumla ya viwanja 1,227 vimepimwa na jumla ya hati 153 zimetengenezwa

**MAENDELEO YA JAMII**

- Vikundi 50 vya wanawake vinavyodaiwa vilifuatiliwa na kuweza kurejesha jumla ya Shilingi 30,327,800.00 kati ya Shilingi 37,379,000.00 ambazo ni sawa na asilimia 81 ya lengo la marejesho.

- Vikundi 24 vya wanawake vimeweza kupatiwa mkopo wenye jumla ya shilingi 21,800,000.00.
- VICOBA 58 vimeweza kuundwa kwenye maeneo mbali mbali ya wilaya ya Magu.
- Uhamasishaji wa ujenzi wa nyumba bora na za bei nafuu ulifanyika kwenye vijiji vya Muda, Matela, Kayenze "B", Isolo, Itandula, Lubugu, Buhumbi, Inonilo, Welamasonga, Nyamahanga, Shinembo, Muda, Sayaka, Ihayabuyaga, Mwamanga, Kisesa, Nyanguge, Salongwe, Igombe na Lugeye.
- Vikundi 36 vya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI vimeweza kufuatiliwa na kuona maendeleo yao na changamoto zinazowakabili.
- Kuratibu kikao kimoja cha mkutano mkuu wa baraza la watu wanaoishi na VVU/UKIMWI kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Macheta tarehe 05/06/2015.
- Mafunzo kwa kamati tendaji za kudhibiti UKIMWI za Vijiji (VMAC) juu ya wajibu na majukumu ya kamati yalitolewa kwa vijiji 8. Vijiji hivyo ni Ilungu, Mwalinha, Shinembo, Kigangama, Kabila, Itumbili, Ng`haya na Nyanguge.

- Vikundi 8 vya Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) viliweza kupewa ruzuku/msaada wa fedha wa jumla ya shilingi 5,000,000.00 kwaajili ya kuendesha shughuli za ujasiriamali kutokana na maombi yao.

- Watoto 77 walio katika mazingira hatarishi wameweza kulipiwa ada ya shule ya Shilingi 2,250,000.00.

- Mafunzo kwa jamii juu ya masuala mbali mbali yanayohusu UKIMWI yamefanyika kwa vijiji 10 kwa kutumia gari la sinema

- Wagonjwa 4 waliotelekezwa Hospitali ya wilaya ya Magu wameunganishwa na ndugu zao. Pia wagonjwa 24 wasio na ndugu wamepatiwa msaada wa chakula, sabuni pamoja na nauli.

- Usuluhishi wa migogoro ya ndoa na masuala ya watoto kesi 271 zimeshughulikiwa. Jumla ya shilingi 1,995,000.00 zimetolewa na wazazi waliotelekeza familia zao kupitia ofisi ya Ustawi wa jamii.

- Walemavu wa ngozi 79 wamepatiwa mafuta ya ngozi jumla ya chupa 288 kwa ajili ya kulinda ngozi zao na madhara yatokanayo na jua.

- Familia 4 za watu wenye ulemavu wa ngozi zimetembelewa na kupatiwa ushauri wa namna ya kuwaendeleza watoto wao wenye ulemavu.

**UTUMISHI NA UTAWALA**

- Vikao 5 vya kisheria vimefanyika kama ilivyopangwa
- Jumla ya watumishi walio masomoni ni 144 kwa mchanganuo ufuatao,afya- 10 Elimu Msingi -77, Ujenzi- 1 Maji-1 Maendeleo ya Jamii- 1, Elimu -sekondari 49 na Utawala -5

- Watumishi mbalimbali wamelipwa madeni yao kadiri fedha zilivyopatikana.

**(d) CHANGAMOTO NA MIKAKATI YAKE**

| NA | CHANGAMOTO | MKAKATI |
|---|---|---|
| 1 | Umaskini wa kipato husababisha uchangiaji duni wa miradi ya maendeleo | Kuwawezesha wanawake na vijana kupata mikopo na elimu ya ujasiriamali. |
| 2 | Ukosefu wa uwazi na usimamizi wa fedha zinazokusanywa katika ngazi ya chini | Kuhamasisha jamii katika dhana ya kushiriki kupanga na kutekeleza shughuli za miradi ya maendeleo |
| 3 | Kuchelewa kuleta fedha za miradi ya maendeleo katika robo ya kwanza na pili | Kuendelea kuikumbusha Serikali kuu kutoa fedha kwa wakati |
| 4 | Kukosekana kwa utaalamu wa masuala ya fedha na manunuzi na usimamizi wa miradi katika ngazi ya Kata na Vijiji | -Kuwajengea uwezo katika masuala ya fedha,usimamizi wa miradi na taratibu za manunuzi<br>-Kuchukua hatua za kisheria kwa wale wanaokiuka taratibu hasa matumizi mabaya ya fedha na pia kutosoma taarifa za mapato na matumiizi kwenye vikao vya kisheria. |

**2.4 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KWA MWAKA 2015/16 (JULAI-DESEMBA) 2015).**

**SEKTA YA MAJI**

.

- Kuendelea na ukukamilishaji wa ujenzi wa mradi wa maji bomba Lugeye-Kigangama kupitia Programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini (RWSSP).
- Uchimbaji wa visima virefu 3 na kufunga pampu za mikono katika vijiji vya Nyan'hanga ,Ng'haya na Lumeji kupitia Programu ya LVEMP-II.

Uchimbaji wa visima virefu 2 na kufunga pampu za mikono katika kijiji cha Ihayabuyaga (Kitongoji cha Njicha na Bukandwe) kupitia Taasisi ya Kanisa la KKKT.

**MIFUGO NA UVUVI**

- Kuongeza kipato kwa wafugaji wa Wilaya ya Magu kwa kuongeza idadi ya minada ya mifugo toka mnada mmoja wa awali kwa sasa hadi mitatu na mnada mmoja wa upili katika Kijiji cha Nyanguge.
- Kupunguza magonjwa ya mifugo na magonjwa yanayo athiri mifugo na binadamu ambapo jumla ya Mbwa 301 walichanjwa dhidi ya ugonjwa hatari wa kichaa cha mbwa, Kuku 118 walipatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa wa Mdondo (NCD), Kuku 1,232 walipatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa wa Ndui na Ng;ombe 146 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa chambavu (BQ).
- Kuwezesha wafugaji nane (8) kushiriki Maonesho ya Nanenane kwa mwaka 2015 yaliyofanyika viwanja vya Nyamhongolo jijini Mwanza ambapo mfugaji bora wa mbuzi wa maziwa alitoka Halmashauri ya Wilaya ya Magu.

- Kufanikisha makubaliano ya kuanzisha mfuko wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika ziwa Victoria.
- Kufanikisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na shughuli za uvuvi ambapo jumla ya Tshs. 11,400,000/= zilikusanywa.
- Uzinduzi wa uvunaji katika mabwawa 7 ya samaki katika kjiji cha Kigangama,Kitongo na Ijinga,jumla ya kilo 660 za samaki zilivunwa zenye thamani ya Tshs 6,414,300=.
- Kufanikisha upandaji wa vifaranga awamu ya pili katika mabwawa 2 yaliyoko katika kijiji cha Ijinga.

**ELIMU SEKONDARI**

- Mitihani ya kidato cha pili, kidato cha nne ilifanyika kama ilivyopangwa.
- Ujenzi wa miundombinu katika shule ya Kahangara umekamilika
- Idadi ya wanafunzi waliofaulu kuingia kidato cha kwanza kwa mwaka 2015 ni **4,539** ambapo wasichana ni **2,263** na wavulana **2,276.**
- Wanafunzi waliofanya mtihani kidato cha pili walikuwa ni **2,634** wavulan**a 1,500** na wasichana **1,134.**
- Wanafunzi waliofanya mtihani kidato cha nne walikuwa **2,495** wavulana **1,308 na** wasichana **1,187**,watahaniwa binafisi walikuwa 147 na watahiniwa 127 walifanya mtihani wa maarifa (Qualifying test)
- Idadi ya vyumba 46 vya maabara vimekamilika bado uwekaji wa samani na mfumo wa gesi

**ELIMU MSINGI**

- Jumla Waalimu **190** wamepewa haki zao za msingi ambazo ni fedha za likizo, matibabu, mazishi uhamisho na gharama za masomo.
- Jumla ya wanafunzi **4539** wamefaulu mtihani wa darasa la saba,na matokeo yalikuwa kama ifuatavyo: wasichana **2263**,Wavulana **2276** ufaulu ni asilimia 81.4% ya jumla ya wanafunzi wote.

- Matarajio ya uandikishaji wa darasa la kwanza ni jumla **13,476**
- Matarajio ya uandikishaji wa darasa la awali ni 11,877
- Uandikishaji wa darasa la MEMKWA ulikuwa kama ifuatavyo- wavulana **990** wasichana **923** jumla **1913** sawa na asilimia **59%**.
- Wanafunzi waliofanya mtihani wa darasa ya nne jumla ni 7,924 (SFNA) Wavulana 3,648,Wasichana 4,276 na waliofanya mtihani wa darasa la nne ni 7,662 Wavulana 3,503,Wasichana 4,159 sawa na asilimia 96.6.
  Jumla ya walimu 860 watapanda madaraja mbalimbali

**SEKTA YA AFYA**

- Haki za watumishi wa afya 140 zimetolewa kwa asilimia 52%
- Vifo vya kina mama wajawazito vimepungua kutoka 131/100,000 mpaka 128/100,000.
- Vifo vya watoto vimepungua kwa asilimia 0.5%.

- Upatikanaji wa dawa ulifikia 80%
- Huduma za afya zimeboreshwa kwa kutoa kinga na tiba kwa ajili ya magonjwa mbalimbali ambapo (Utoaji Chanjo umefikia 100
- Ugonjwa wa malaria umepungua kwa asilimia 5%
- Mfuko wa bima ya afya umeongezeka kwa asilimia 5%

**KILIMO NA UMWAGILIAJI**

- Mashamba darasa 90 ya zao la mahindi ya mbegu zinazokabiliana na kiduha yameanzishwa katika vijiji vya Mwalinda,Mwamabanza na magu mjini.
- Ukarabati wa malambo kwa utaratibu wa chakula kwa kazi (Food for work) umefanyika katika vijiji vya Mwalinha na Kinango.
- Usimamizi wa usambazaji wa mbegu za pamba umefanyika katika vijiji vyote vinavyolima pamba Wilayani.
- Wilaya imeshiriki katika maonesho ya NaneNane 2015 ambayo yamefanyika Kikanda katika uwanja wa Nyamohongholo Mwanza
- Ushauri umetolewa kwa wakulima 120,000 wa zao la pamba wilani kuhusu kuanza kutekeleza mapema maandalizi ya kilimo msimu 2015/16.
- Wakulima wa mbegu katika daraja la kuazimiwa wametambuliwa na kupatiwa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu katika vijiji 14.
- Watumishi 66 wamepewa mafunzo ya kilimo biashara.
- Skimu 8 za umwagiliaji zimepewa mafunzo juu ya utunzaji na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji.

**MIPANGO TAKWIMU NA UFUATILIAJI**

- Mafunzo ya PLANREP yametolewa kwa watumishi 14
- Miradi ya mwenge imeratibiwa kikamilifu.
- Usimamizi na ufuatiliaji wa Miradi katika kata 25 umefanyika.
- Vijiji 82 viliwezeshwa kuibua viapaumbele vyao kupitia Mfumo wa Fursa na Vikwazo (O & OD).
- Mfumo wa takwimu umeboreshwa na takwimu zimehuishwa.

**MAENDELEO YA JAMII**

- Vikundi 9 vya wanawake vinavyodaiwa vilifuatiliwa na kuweza kurejesha jumla ya Shilingi 2,039,600.00.

- Vikundi 5 vya wanawake vimeweza kupatiwa mkopo wenye jumla ya shilingi 5,000,000.00.
- Kuratibu maonesho ya vikundi 17 vya ujasiriamali vya wanawake siku ya kilele cha mbio za mwenge tarehe 25/08/2015.
- Usuluhishi wa migogoro ya ndoa na masuala ya watoto kesi 45 zimeshughulikiwa. Jumla ya shilingi 1,270,000.00 zimetolewa na wazazi waliotelekeza familia zao kupitia ofisi ya Ustawi wa jamii.

- Wagonjwa 3 waliotelekezwa Hospitali ya wilaya ya Magu wameunganishwa na ndugu zao. Wagonjwa hao wanatoka kwenye maeneo ya Bariadi, Buhumbi na Busega.

- Mashirika yanayojaza fomu ya TOMSHA yapatayo 5 yaliweza kufuatiliwa na kuleta fomu zao walizojaza. Mashirika hayo ni MAGU YOUTH DEVELOPMENT NETWORK (MAYODEN), WATU WANAOISHI NA VVU (WAWAVUMA), RAFE, UVUUMA na MAPERECE.

- Uhamasishaji kwa jamii juu ya upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa kata za Kisesa, Bujora, Bujashi na Bukandwe. Uhamasishaji huu ulifanyika kwenye wiki ya siku ya mwenge na mkesha wake katika kijiji cha Kisesa tarehe 25 August 2015.
- Vikundi 8 vya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI vimeweza kufuatiliwa na kuona maendeleo yao na changamoto zinazowakabili.

**MALIASILI NA ARDHI**

- Jumla ya miti 434,562 imepandwa wakati wa mvua.
- Doria 6 zimefanyika katika vijiji vinavyozunguka hifadhi ya msitu wa Sayaka, hii ni sawa na asilimia 50 ya doria zilizopangwa kufanyika.
- Mizinga ya kisasa 615 imetengenezwa na kutundikwa chini ya Ufadhili wa mradi wa LVEMP II na TaFF
- Mafunzo juu ya ufugaji nyuki na utunzaji wa mazingira yametolewa kwa vikundi 8 vinavyojishulisha na ufugaji kupitia kupitia miradi ya TaFF na LVEMP II.
- Jumla ya viwanja 915 vimepimwa maeneo ya magu mjini,Isangijo na Kisesa
- Jumla ya hati 162 zimetengenezwa

## MPANGO NA BAJETI YA HALMASHAURI KWA MWAKA 2016/17

Katika kuandaa bajeti ya mwaka 2016/17 mambo muhimu yaliyozingatiwa ni kama ifuatavyo**:-**

- Halmashauri imejikita katika miradi inayolenga kuleta matokeo makubwa sasa yaani BRN kupitia sekta zilizoainishwa.
- Halmashuri kutoanzisha miradi mingine mipya kabla haijakamilisha miradi ya kipindi kilichopita (Miradi Viporo)
- Halmashauri imejikita katika miradi inayolenga kukuza uchumi na kupunguza umaskini (MKUKUTA)
- Ushirikishwaji wananchi na wadau wa maendeleo katika kuandaa na kutekeleza miradi ya maendeleo pia shughuli za kawaida zinazowagusa maisha yao.
- Mpango na bajeti ya Halmashauri umezingatia masuala ya mtambuka kama vile ushirikishwaji wananchi na wadau masuala ya Jinsia, mazingira, vijana, ukimwi na kuzuia rushwa.
- Kuzingatia Ilani ya Chama Tawala (CCM), ahadi mbalimbali za viongozi wa kitaifa, Dira ya maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, Mpango wa miaka mitano wa Wilaya na sera za sekta mbalimbali.
- Miradi viporo ya Mwaka 2013/14 na 2014/15 inawekwa kwenye bajeti ya mwaka 2016/17

- Kutekeleza mpango wa D by D (ugatuaji wa madaraka na raslimali fedha) kwa kutenga fedha za kujenga uwezo kwa mamlaka za serikali ngazi ya chini (empowering lower level )
- Hotuba ya Mh Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

## 1.3 VIPAUMBELE VYA BAJETI YA MWAKA 2016/17

### SEKTA YA ELIMU MSINGI

- Kuongeza kiwango cha ufaulu kutoka asilimia 81.39% kwa darasa la saba kwenda 85%.ifikapo Juni 2017.
- Kupunguza uhaba wa madarasa kutoka 887 hadi 863 kwa Kujenga vyumba 24 vya madarasa.ifikapo juni 2017
- Kupunguza uhaba wa nyumba za walimu kutoka 1166 hadi 1162 kwa Kujenga nyumba 4 ifikapo 2017
- Kupunguza uhaba wa matundu ya vyoo kutoka 2909 hadi 2809 kwa Kujenga matundu ya vyoo 100 ifikapo juni 2017.
- Kupunguza uhaba wa madawati kutoka 26,453 hadi 25953 kwa Kutengeneza madawati 500 ifikapo juni 2017
- Kupunguza uhaba wa walimu kutoka 465 kwa sasa hadi walimu 232 ifikapo Juni 2017 kwa Kuajiri walimu 233.
- Kuwalipa waalimu fedha za likizo ,Matibabu na huduma ya mazishi
- Jumla ya walimu 303 wanatarajia kupanda madaraja mablimbali

### SEKTA YA ELIMU SEKONDARI

- Kuongeza kiwango cha ufaulu kidato cha sita kutoka asilimia 86% kwa sasa hadi 90%.ifikapo Juni 2017
- Kuongeza kiwango cha ufaulu kidato cha nne kutoka asilimia 73% kwa sasa hadi 82% Ifikapo Juni 2017.
- Kuongeza kiwango cha ufaulu kidato cha pili kutoka asilimia 91% kwa sasa hadi 97%. ifikapo Juni 2017.
- Kupunguza uhaba wa nyumba za walimu kwa Kujenga nyumba 18 za waalimu.
- Kuweka umeme katika shule za sekondari 5 kati 18
- Kupunguza uhaba wa walimu kutoka 166 hadi 106 kwa kuajiri walimu 60 wa masomo ya sayansi na Hisabati
- Kupunguza uhaba wa matundu ya vyoo kutoka 518 hadi 422.kwa kujenga matundu 96
- Kuweka samani na mfumo wa gesi katika vyumba 46 vya maabara.
- Kuchimba visima vifupi 3 vya maji katika shule 3 sekondari
- Kuongeza madarasa ya elimu ya sekondari ya juu kwa kujenga vyumba vinne vya madarasa katika shule za sekondari kabila na kitumba.
- Kuwalipa waalimu fedha za likizo ,Matibabu na huduma ya mazishi

### SEKTA YA MAJI

- Kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama katika ngazi ya vijiji kutoka asilimia 43 kwa sasa hadi 55% hasa kwenye vijiji kumi vilivyoainishwa ifikapo Juni 2017.
- Kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama Magu mjini kutoka asilimia 22% kwa sasa hadi asilimia 43% ifikapo Juni 2017.
- Kuchimba visima virefu 75 na kufunga pampu za mikono katika kata zote za Halmashauri
- Kuwalipa watumishi fedha za likizo ,Matibabu na huduma ya mazishi

**SEKTA YA MIFUGO**

- Kupunguza matukio ya magonjwa na vifo kwa Mifugo kutoka 25% kwa sasa hadi 22% ifikapo Juni 2017.
- Kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao yatokanayo na mifugo, uzalishaji wa Maziwa kwa ng'ombe wa asili toka 0.5 kwa mkamuo kwa siku kwa sasa hadi lita mbili (2) kwa mkamuo ifikapo juni 2017. Vilevile kuongeza uzalishaji wa Nyama kutoka kilo 70 kwa ng'ombe kwa sasa hadi kilo120 na uzalishaji wa ngozi kutoka kilo tatu (3) kwa ngozi kwa mnyama kwa sasa hadi kilo tano (5) ifikapo juni 2017.
- Kuboresha huduma za ugani wa shughuli za mifugo Wilayani kutoka 80% kwa sasa hadi 85% ifikapo juni 2017.
- Kukusanya mapato yatokanayo na leseni za mitumbwi na wavuvi kutoka Shilingi 36,000,000/= kwa sasa hadi Shilingi 40,500,000/= ifikapo Juni 2017.
- Kuongeza ufanisi wa utendaji wa BMU 8 kwa kufanya chaguzi hadi ifikapo juni 2017.
- Kutoa elimu ya ufugaji wa samaki katika mabwawa kwa wafugaji wa samaki wa vijiji vine (4) na kuwasaidia wafugaji wa samaki wapya 20 hadi ifkapo Juni 2017.

- Kuwalipa watumishi fedha za likizo ,Matibabu na huduma ya mazishi

**SEKTA YA KILIMO NA UMWAGILIAJI**

- Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani 85,599 hadi 89,879 ikikapo juni 2017
- Kuongeza uzalishaji wa mbegu katika daraja la kuazimia kutoka 0 hadi tani 14.4% ikfikapo juni 2017.
- Kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara kutoka tani 18,574.6 hadi tani 19,503.3 ikfikapo juni 2017
- Kuongeza hekta za umwagiliaji kutoka hekta 150 za sasa hadi 220 ifikapo 2017.

**ARDH INA MALIASILI**

- Kuboresha uoto wa asili kwa kuimarisha doria na kusimamia Sheria ya utunzaji wa mazingira na kuimarisha vikundi vya wafugaji nyuki.
- Kuweka mpangilio mzuri wa miji ya Magu, Kisesa na mji mingine midogo ya Nyanguge, Kabila, Lugeye, Mahaha na Sukuma.
- Kuwalipa watumishi fedha za likizo ,Matibabu na huduma ya mazishi
- Jumla ya viwanja 2,057 vinatarajiwa kupimwa
- Jumla ya Hati 350 zitatengezwa
- Kuandaa mpango wa jumla wa wilaya wa matumizi ya ardhi(General land use plan)
- Kuanzisha vitalu 2 vya miche 4,134 mbalimbali
- Kuendeleza misitu 4 ya Halmashauri ya wilaya ya Magu.

**UTAWALA BORA**

- Kupunguza uhaba wa ofisi za vijiji kwa Kujenga Ofis 5 za vijiji

- Kuratibu na kusimamia uchaguzi Mkuu wa Madiwani, Wabunge na Rais.
- Kusimamia utekelezaji wa utawala bora kwa vitendo kwa kusimamia vikao vya kisheria katika ngazi zote
- Kuwalipa watumishi fedha za likizo ,Matibabu na huduma ya mazishi
- Kuratibu shughuli za nanenane, na masuala ya Mbio za Mwenge wa uhuru.

**MAENDELEO YA JAMII**

- Kusaidia Kukuza Ajira Kwa Vijana na Kina Mama kwa kusaidi mtaji wa kiasi cha Tshs 40,000,000/= ifikapo Juni 2017
- Kushirikiana na asasi mbalimbali kupunguza maambukizi ya UKIMWI toka 6.02% hadi 5% ifikapo Juni 2017.
- Kuwalipa watumishi fedha za likizo, Matibabu na huduma ya mazis**hi.**
- Kupunguza matendo ya unyanyasaji wa kijinsia na ukatili kwa watoto kwa asilimia 10 kutoka 48% hadi 38% ifikapo Juni 2017.
- Kuboresha maslahi ya wazee na watu wenye ulemavu
- Kuwezesha kitengo cha vijana vitendea kazi
- Kuendeleza kituo cha makumbusho Lugeye

**SEKTA YA AFYA**

- Kuboresha utoaji wa huduma ya kinga kutoka 94% kwa sasa hadi 97%
- Kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI kutoka asilimia 4.2% kwa sasa hadi 2.5% ifikapo Juni 2016.
- Kuboresha utoaji wa huduma ya afya ya mama na mtoto kutoka 88% kwa sasa hadi 92% ifikapo Juni 2016.
- Kukamilisha vituo 4 vya afya na Zahanati 3 ifikapo Juni 2016.
  Kupunguza vifo vya kina mama na watoto kutoka 137/100,000 hadi 124/100,000
- Kuwalipa watumishi fedha za likizo ,Matibabu na huduma ya mazishi

Kwa mwaka wa fedha 2016/17 Halmashauri inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tshs. **33,055,415,488** **kutoka** vyanzo vyake mbalimbali na kutoka ruzuku ya Serikali Kuu kama ifuatavyo:-

| **Chanzo cha fedha** | **Makisio 2015/2016** |
|---|---|
| Mishahara | 21,761,126,738 |
| Matumizi mengineyo | 1,565,695,000 |
| Miradi ya maendeleo na Wahisani | 7,526,916,000 |
| Mapato ya ndani | 1,798,366,750 |
| Ruzuku Maalumu | 403,311,000 |
| GPG | |
| **JUMLA KUU** | **33,055,415,488** |

**4.0 MAOMBI MAALUMU NJE YA BAJETI KWA MIRADI YA MAENDELEO**

Kutokana na ukomo wa bajeti kuwa finyu ukilinganisha na mahitaji yaliyopo, Halmashauri inakusudia kuomba jumla ya Tshs. **6,936,740,333.00** kwa ajili ya miradi ya Maendeleo kama ifuatavyo:-

**(a)MIRADI INAYOENDELEA**

Miradi inayoendelea imepewa fedha Kama ifuatavyo:-

| NA | JINA LA MRADI | JUMLA YA GHARAMA YA MRADI | FEDHA ZILIZOTOLEWA | FEDHA ZINAZOOMBWA 2015/2016 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri | 1,759,486,805.34 | 726,626,651 | |
| 2 | Ujenzi wa mradi maji bomba Nsola Bubinza | 1,379,485,195 | 20,000,000 | 1,359,485,195 |
| 3 | Kufanya usanifu wa miradi ya maji kusimamia ujenzi na kujitengea uwezo jamii katika vijiji 10 awamu ya pili mkataba | 358,182,723.00 | 213,385,213.86 | 144,797,509.14 |
| 4 | Ukarabati wa visima 10 visima virefu 15 na kutoa mafunzo kwa kamati za watumiaji maji katika kata za Kahangala,,Sukuma,,Nghaya,,Nyangunke, Mwamabanza na Nkungulu | 357,612,000 | 170,740,000 | 170,740,000 |
| 5 | Ujenzi wa mradi wa maji bomba Nyanguge(Ujenzi wa chanzo cha maji,ujeniz wa matanki yenye kubwa wa mita za ujazo 225 na ufungaji wa dira za maji | 1,347,233,468 | 1,270,693,844 | 76,539,624 |
| **JUMLA** | | **3,457,297,044** | **374,000,000** | **3,207,297,044** |

(**b)MIRADI MIPYA**

| NA | JINA LA MRADI | GHARAMA KWA KILA MRADI |
|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Miundo mbinu ya maji kwenye Kata ya Ng,haya | 1,500,300,000 |
| 2 | Ujenzi wa Hosteli ya wasichana maeneo ya pembezoni | 600,000,000. |
| 3 | Ujenzi wa stendi ya mabasi na maegesho ya Malori makubwa Kisesa | 1,500,000,000 |
| **JUMLA** | | **3,600,300,000** |

**Jumla ya Maombi Miradi Mipya…….....Tsh 3,108,654,389./=**

**Jumla ya Maombi Kwa miradi yote …….Tsh 6,315,651,433/=**

Jumla ya A+B= **6,315,651,433** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uidhinishe Fedha za Bajeti ya kawaida **33,055,415,488** na Maombi Maalumu kwa Miradi ya Maendeleo Tshs. **6,315,651,433** na kufanya jumla ya Tshs. **39,371,066,921** kwa ajili ya Halmashauri ya Magu.